

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL  
Kenya Certificate of Secondary Education

102/3

— KISWAHILI — Karatasi ya 3  
FASIHI

Nov. 2019 – Muda: Saa 2½



Jina ..... Nambari ya Mtahiniwa .....

Sahihi ..... Tarehe .....

Maagizo

- (a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.  
(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.  
(c) Jibu maswali **manne** pekee.  
(d) Swali la kwanza ni la **lazima**.  
(e) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani:  
Tamthilia, Hadithi Fupi, Ushairi na Fasihi Simulizi.  
(f) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.  
(g) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.  
(h) Majibu yote **sharti** yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.  
(i) **Karatasi hii ina kurasa 24 zilizopigwa chapa**.  
(j) **Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	
Jumla		



919294



## SEHEMU A: RIWAYA

### A. Matei: *Chozi la Heri*

#### 1. Lazima

- (a) “Sasa haya ameyapa kisogo ... kufunguliwa kwa kituo hiki ni kama mana iliyomondoklea kinywani kutoka mbinguni.”
- (i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  - (ii) Bainisha tamathali **mbili** za usemi ambazo zimetumiwa katika dondoo hili. (alama 2)
  - (iii) Fafanua umuhimu wa mhusika anayerejelewa katika dondoo hili katika kuijenga riwaya hii. (alama 6)
- (b) Jadili mikakati mwafaka ambayo vijana wanatumia kukabiliana na hali yao ya maisha kwa kuwarejelea wahusika wafuatao:
- (i) Chandachema (alama 4)
  - (ii) Dick (alama 4)

## SEHEMU B: TAMTHILIA

### P. Kea: *Kigogo*

*Jibu swali la 2 au la 3*

2. (a) Jadili mbinu **kumi** ambazo Wanasa gamoyo wanatumia kupigana na utawala dhalimu. (alama 10)
- (b) Eleza jinsi mbinu rejeshi ilivyotumiwa kukuza vipengele vifuatavyo katika tamthilia hii.
- (i) Maudhui (alama 5)
  - (ii) Wahusika (alama 5)
3. (a) “Ushahidi utatoka wapi kama kipanga ndiye hakimu kwenye kesi ya kuku?”
- (i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  - (ii) Fafanua dhima ya vipengele **viwili** vya kimtindo vinavyobainika katika dondoo hili. (alama 4)

- (b) (i) Kwa kurejelea tamthilia jadili sifa **sita** za msemaji. (alama 6)
- (ii) Eleza umuhimu wa mandhari katika tamthilia hii. (alama 6)

### SEHEMU C: HADITHI FUPI

*Jibu swali la 4 au la 5*

**A. Chokocho na D. Kayanda (Wah): Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine**

*K. Walibora: "Nizikeni Papa Hapa"*

4. (a) "Isije ikawa hapa habari ya kufuata asali ukafa mzingani." "... Pana hasara gani nzi kufia kidondani?"
- (i) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 5)
- (ii) Andika mbinu **mbili** za kimtindo zinazojitokeza katika dondo hili. (alama 2)
- (b) Hadithi, *Nizikeni Papa Hapa* inahimiza uwajibikaji. Jadili. (alama 6)
- (c) Eleza jinsi maudhui ya umaskini yanavyojitokeza katika hadithi, *Mapenzi ya Kifaurongo.*" (alama 7)

*A. Chokocho: "Shogake Dada ana Ndevu"*

5. (a) Onyesha jinsi unafiki unavyoshughulikiwa katika hadithi, "*Shogake Dada ana Ndevu.*" (alama 8)
- (b) Changanua mtindo katika dondo lifuatalo: (alama 12)

"Bi. Hamida alitunga donge kifuani mwake. Na donge likaja juu. Likampanda na kumsakama kooni. Kweli? Uongo? Kweli au uongo yale maneno ya binti yake? Labda kweli anamfikiria mambo mabaya binti yake tu. Labda kweli dhana yake ni mbovu. Bi. Hamida alichanganyikiwa na mambo. Alivutwa huku na huku na nafsi yake yenye chagizo. Upande mmoja sauti yake ya ndani ilikuwa inamtetea Safia, na upande wa pili wa nafsi yake ilikuwa ikimshuku Safia; na sauti zake zote mbili hizo zimo ndani ya kiwiliwili chake zinamvuta yeye mtu mmoja, Bi. Hamida. Hatimaye hakutambua afanye nini."